



JOHN MERLANI SECONDARY SCHOOL

MISSIONARIES OF THE PRECIOUS BLOOD
P.O. Box 2010
DODOMA – TANZANIA

tel. 0766 939 536
e-mail: imerlinisec@gmail.com
web-site: cppseducationtz.org

Registration N° S 4880, NECTA Exams N° S 5391

Picha yako

FOMU YA OMBI LA KUJIUNGA NA SHULE 2019

Shule ya Sekondari ya John Merlani ipo Miyuji, Manispaa ya Dodoma. Inamilikiwa na Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi. **Ni shule ya mseto, wasichana kwa wavulana, na ya bwani.**

Fomu za ombi la kujiunga na shule kwa mwaka 2019 zinatolewa shuleni John Merlani na katika Parokia za Kisasa, Kanisa Kuu, Radio Mwangaza (Dodoma) na Parokia za Mtongani, Bahari Beach, Boko, St. Gaspar Mbezi Beach, Tegeta (Dar es Salaam) na Parokia ya Damu Azizi (Kola, Morogoro). Gharama ya Form ni sh. 15,000/- Gharama ilipwe kwa njia ya benki. Siku ya mtihani wa kujiunga na shule mwanafunzi aje na pay in slip ya benki ili aruhusiwe kufanya mtihani. Atapata risiti ya shule:

- JINA LA BANK: **NMB**
- JINA LA ACCOUNT: **JOHN MERLANI SECONDARY SCHOOL**
- NAMBA YA ACCOUNT: **52010026469**

Mtihani wa kujiunga na shule (entrance test) utafanyika shuleni John Merlani (Dodoma), katika Chuo cha Mt. Gaspari, Kola (Morogoro) na katika chuo cha St. Gaspar, Mtongani (Dar es Salaam), Jumatatu tarehe **17/9/2018** kuanzia saa 2:00 asubuhi. **Wanachaguliwa kujiunga na shule mwaka 2019 wale tu waliopasi mtihani wa kuingia (entrance tests) kwa alama isiyo chini ya 27 katika kila somo.**

Wote wanaoingia J. Merlani mwaka 2019 lazima wasome Pre Form I. Masomo yataanza tarehe 1/10/2018, yatakwisha tarehe 30/11/2018 na yatakwepo kila siku ya Jumatatu hadi Ijumaa, kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi 11:30 jioni. Kifungua kinywa na chakula cha mchana vitatolewa shuleni. Karo ya masomo ya Pre Form I ni sh. 80,000 kwa mwezi. Gharama hii nayo ilipwe kwa njia ya benki. Kwa wanaotoka nje ya Dodoma nafasi ya bwani ipo kwa sh. 70,000 kwa mwezi.

Ada ya mwaka 2019 (shule, bwani, michango) ni jumla sh. milioni mbili (2,000,000), michango ikiwemo ndani. Inaweza kulipwa kwa awamu moja (January siku shule inapoanza) au awamu mbili (January na July) au awamu tatu (January, Aprili, July). Ada yote ilipwe ndani ya mwezi July. Malipo ni kwa njia ya Benki.

Urudishe fomu hii aidha kabla yasiku ya mtihani au siku yenyewe ya mtihani wa kujiunga na shule.

Maelezo:

Jina la Mwanafunzi

Jina la Baba Mzazi/Mlezi

Jina la Mama Mzazi

Tarehe – Mwezi – Mwaka wa kuzaliwa

Mwaka wa kumaliza elimu ya msingi

Shule ulipomaliza elimu ya msingi

Simu ya Mzazi/Mlezi wako Tarehe